# MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI MENEJIMENTI (C.M.T) KILICHOFANYIKA TAREHE 15.12.2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILINDI.

**WAKUU WA IDARA NA VITENGO WALIOHUDHURIA:**

1. Gracian Makota - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Wilaya
2. Rashidi Abeid - Kaimu Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala
3. Mary S. Muhoza - Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Ufuatiliaji
4. Emmanuel S.Mnanka - Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili
5. Ulirch P. Laswai - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA
6. Senasy B. Joseph - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
7. Suleimani Mwarabu - Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi
8. Innocent Nsojo - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi
9. Aquilina Xavery - Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii
10. Dr. Lukemelye Mwenga - Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya
11. Arapha Baraza - Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara
12. Rodgers D. Shemahonge - Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira
13. Gordian Gwiyago - Mkuu wa Idara Kilimo, Umwagiliaji Ushirika
14. Adam Sylvester - Mkuu wa Kitengo cha Nyuki
15. Phoibe Ngereza - Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi
16. Rickson Jackson - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria
17. Mbonea Mfinanga - Mratibu TASAF
18. Aloyce Mhando - Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi
19. Clovis Mrutu - Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi
20. Laura Samwel - Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi
21. Neema K. Kabura - Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari

**WAKUU WA IDARA NA VITENGO WASIOHUDHURIA:**
Hakuna

**MWANDISHI WA KIKAO.**

1. Zedrick Chisongela - Mwandishi wa Mikutano
2. Caster Mahimbo - Mwandishi wa Mikutano

**CMT.MUHT.NA.1/12/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO.**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afungue kikao baada ya akidi kutimia, kabla ya kufungua kikao Mwenyekiti aliwasalimia wajumbe na aliwakaribisha kwenye kikao kisha alifungua kikao mnamo saa 5:24 asubuhi.

**CMT.MUHT.NA.2/12/2021/2022: KUTHIBITISHA AGENDA.**

Wajumbe walizithibitisha na kuzipokea jumla ya agenda 12 za kikao ambazo ni:-

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda

3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha kamati ya Menejimenti cha tarehe 17.11.2021
4. Yatokanayo na kikao cha Kamati ya Menejimenti cha tarehe 17.11.2021
5. Kusoma muhtasari na maazimio ya kikao cha kamati ya fedha, uongozi na mipango cha tarehe 19.11.2021
6. Taarifa ya mapato na matumizi ya mwezi Novemba 2021
7. Mapendekezo ya kutumia serikali za vijiji kwenye ukusanyaji wa mapato
8. Mchanganuo wa Fedha za UVIKO 19
9. Taarifa ya Uanzishwaji wa Kituo cha Matangazo ya Redio
10. Taarifa ya Mapendekezo ya Mikopo (utoaji) kutoka kwenye kamati ya Huduma za Mikopo
11. Mengineyo
12. Kufunga kikao.

**CMT.MUHT.NA.3/12/2021/2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA MENEJIMENTI CHA TAREHE 5.10.2021**

Muhtasari ulisomwa na kufanyiwa maboresho mwisho Katibu na Mwenyekiti waliusaini kuwa ni kumbukumbu sahihi ya kikao.

**CMT.MUHT.NA.4/12/2021/2022: YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAMATI YA MENEJIMENTI CHA TAREHE 5.10.2021**

Maazimio yaliwasilishwa na wajumbe waliridhia kuwa Azimio linalohusu Ukaguzi katika shule ya Msingi Ngeze wa ujenzi matundu ya vyoo liwasilishe kwenye kikao kijacho cha kamati ya Fedha. Aidha waliridhika na utekelezaji wa maazimio mengine.

**CMT. MUHT. NA. 5/12/2021/2022: KUSOMA MUHTASARI NA MAAZIMIO YA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 19.11.2021**

Muhtasari ulisomwa na kufanyiwa marekebisho mbalimbali ili kuborehwa kwa ajili ya kuingizwa kwenye kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.
Kuhusu suala la matundu ya vyoo katika shule ya Msingi Ngeze wajumbe waliziagiza idara za Elimu Msingi, Mipango, Ujenzi pamoja na Kitengo cha Manunuzi wakakae na wahusika ili kuona namna bora ya kufanya ili kukamilisha mapungufu yaliyojitokeza kwa ajili ya kufuta hoja hii.

**CMT. MUHT. NA. 6/12/2021/2022:TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWEZI NOVEMBA 2021.**

Mkuu wa Idara ya Fedha aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi ya mwezi Novemba 2021/2022 ambapo hadi kufikia tarehe 30 Novemba 2021 Halmashauri imepokea na kukusanya jumla ya Tsh **9,264,645,176.99** Sawa na 31.68% ya makisio ya Tshs **29,242,468,953.00.00** kwa mwaka. Mapato hayo yamekusanywa na kupokelewa katika vyanzo vifuatavyo:-

| MCHANGANUO WA MAPATO KWA MUHTASARI | | KIASI |
|---|---|---|
| **VYANZO MBALIMBALI VYA HALMASHAURI** | | |
| • Vyanzo vya ndani<br>• Uchangiaji huduma za afya<br>• **Uchangiaji ada mashuleni**<br>**Jumla Ndogo** | **Tshs.** 510,448,905.49<br>**Tshs. 113,245,270.00**<br>**Tshs.20,895,500.00** | **644,589,675.49** |
| **RUZUKU TOKA SERIKALI KUU** | | |
| • Mishahara<br>• Matumizi mengineyo (OC)<br>**Jumla ndogo** | **Tshs.6,723,726,789.84**<br>**Tshs. 274,789,717.66** | **6,998,496,507.50** |
| • Miradi ya maendeleo serikali kuu (Local) | Tshs. | **1,395,374,994.00** |
| • Miradi ya maendeleo ya wahisani (Foreign) | Tshs. | **226,184,000.00** |
| **JUMLA NDOGO** | | **1,621,558,994.00** |
| **JUMLA KUU TSHS.** | | **9,264,645,176.99** |

Hadi kufikia Mwezi Novemba 2021, vyanzo vya ndani vya Halmashauri vimekusanya jumla ya Tshs 644,589,675.49 Sawa na **25.19%** ya Makisio ya **Tshs. 2,558,594,250.00** Kwa mwaka, Kwa mchanganuo ufuatao, Mapato ya vyanzo vya ndani halisi **Tshs. 510,448,905.00 sawa na asilimia 25.33 ya makisio ya Tshs.2,015,494,250.00** Na uchangiaji WA huduma za Afya Na Ada Ni Ths **134,140,770.00** sawa na 24.6% ya makisio ya Tshs **543,000,000.00**

Kwa Mwezi Novemba pekee tumekusanya Jumla ya Tshs **97,211,796.50** sawa na 3.8% ya Makisio kwa mchanganuo ufuatao,vyanzo vya ndani Halisi Makusanyo ni **85,921,676.50** na vyanzo lindwa ni Tshs **11,290,120.00** sawa na **2%** ya makisio ya tshs **543,000,000.00**

Halmashauri imepokea fedha nje ya bajeti zenye jumla ya Tshs 433,231,075.51 Ikiwa ni fedha za Miradi kama ifuatavyo:-

- Ujenzi wa nyumba ya Mganga Tshs 90,000,000.00
- Ujenzi wa Emergency Medical Dept Tshs 300,000,000.00
- Fedha za chanjo awamu ya pili Tshs 36,731,075.51
- Fedha za ufuatiliaji wa miradi ya UVICO Tshs.6,500,000.00

**MATUMIZI**

Makisio Kwa mwaka 2021/2022 ni jumla ya Tshs **29,242,468,650**, mpaka mwezi Novemba 2021, Halmashauri imetumia jumla ya **Tshs 8,747,954,032.76** Sawa na **31.68%** ya makisio kwa mwaka, mchanganuo wa matumizi ni kama ifuatavyo:

| NA | MCHANGANUO WA MATUMIZI KWA MUHTASARI | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | **VYANZO MBALIMBALI VYA HALMASHAURI** | |
| | • Matumizi ya kawaida Tshs. **326,262,721.00**<br>• Kuchangia own source Dev. Tshs. **68,095,000.0**<br>• Kuchangia huduma za afya Tshs.**50,445,000.00**<br>**Jumla ndogo** | **434,803,221.00** |
| 2. | **RUZUKU TOKA SERIKALI KUU** | |
| | • Mishahara Tshs. **6,755,511,257.76**<br>• Matumizi mengineyo OC Tshs. **176,392,497.00**<br>**JUMLA MISHAHARA,OC** | **6,931,903,754.76** |
| 3. | • Miradi ya maendeleo serikali kuu (local) Tshs.0 | **1,395,374,994.00** |
| 4. | • Miradi ya maendeleo ya wahisani (Foreign) Tshs.0 | **226,184,000.00** |
| | **Jumla kuu** **Tzs.** | **8,747,954,032.76** |

Ruzuku ya kuendesha ofisi na Mishahara ina makisio ya Tshs **19,446,690,400.00** Kwa mwaka. Hadi mwezi **Novemba**, zimetumika jumla ya Tshs. **6,931,903,754.76** sawa na **35%** ya makisio kwa mwaka. Aidha kwa mwezi **Novemba** pekee zimetumika Tshs **1,341,499.92** sawa na 7% ya Makisio kwa mwaka.

**Miradi ya MAENDELEO**

Chanzo hiki kuna jumla ya Makisio ya Tshs 7,237,184,300. Hadi kufikia mwezi Novemba ,Matumizi yana jumla ya Tshs 1,371,558,994.00 yametumika Sawa na 33.37% ya makisio ya Miradi.

**BAKAA**

| NA. | CHANZO CHA FEDHA | KIASI KILICHOBAKI | KIASI KILICHOTUMIKA | SALIO HADI SASA |
|---|---|---|---|---|
| | MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI | 18,679,013.82 | 18,676,013.82 | 0 |
| | MFUKO WA AFYA (Basket Fund – HSBF) | 152,800,142.27 | 152,800,142.27 | 0 |
| | GLOBAL FUND | 5,261.46 | 5,261.46 | 0 |
| | CENTRAL GOVERNMENT OTHER SOURCE | 58,530,266.48 | 50,000,000.00 | 8,530,266.48 |
| | CAPITATION GRANTS-DEV | 33,238,227.31 | 33,238,227.31 | 0 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | PROGRAMME FOR RESULTS – P4R | 154,885,200.18 | 154,885,200.18 | 0 |
| | POSHO YA MADARAKA (RESPONSIBILITY GRANTS) | 13,700,000.00 | 13,700,000.00 | 0 |
| | FIDIA YA ADA(SCHOOLS FEE COMPENSATION) | 4,848,603.69 | 4,848,603.69 | 0 |
| | MAHITAJI MAALUM (SPECIAL NEEDS SCHOOL GRANTS) | 6,879,669.79 | 6,879,669.79 | 0 |
| | TANZANIA EDUCATION AUTHORITY (TEA) | 33,532,096.44 | 30,000,000.00 | 3,532,096.00 |
| | CHAKULA CHA WANAFUNZI (SCHOOL MEALS GRANTS) | 4,114,375.16 | 4,114,375.16 | 0 |
| | OTHER DEVELOPMENT GRANTS- LOCAL | 56,124,221.00 | 56,124,221.00 | 0 |
| | **JUMLA KUU TSHS** | **537,337,077.60** | **525,274,714.52** | **12,062,362.48** |

Tulivuka na Bakaa ya jumla ya Tshs 537,337,077.60 hadi kufikia Nobemba 30 jumla ya Tshs 525,274,714.52 zimetumika sawa na 98% ya pesa zilizovuka Mwaka.

**CHANGAMOTO:-**

- Hali ya Mapato bado hairidhishi,kwani hadi oktoba tulipaswa tuwe na asilimia 33.3 lkn tumekuanya asilimia 21.3 tupo nyuma kwa asilimia 12
- Hali ya Mfumo wa Mapato bado haujakaa vizuri,hivyo kudhoofisha ufuatiliaji wa Mapato kwa wakusanyaji na kuweza kubaini kiasi halisi kilichokusanywa
- Uchakavu wa vitendea kazi,kwani tumekuwa tukufanya marekebisho ya mara kwa mara ili tuweze kuwa na magari ya kwenda nayo vijijini ,matokeo yake tunatumia gharama nyingi kufufua gari,na gari halidumu ktk matengezezo

**UTATUZI**

- Menejiment imejipanga kufanya ufuatiliaji wa wa Mapato kupitia wakuu wa idara wenyewe pasipo kuwakilishwa.ki makundi kama jinsi Ratiba hiyo ilivoambatanishwa
- Menejiment pia imejipanga kwa kila mkuu wa idara mwenye vyanzo vya kusimamia,ahakikishe anasimamia kikamilifu ukuswanywaji wa Mapato hayo na kuingizwa kwenywe machine za kukusanyia

- Menejiment inaendelea kufanya mawasiliano na wataalamu wa mifumo ili kuhakikisha mifumo ya Mapato inatengemaa na kuleta ufanisi katika kazi
- Menejimenti, inaendelea kufuatilia Magari ambayo tayari yameshalipiwa,kuhakikisha yanakuja kuongeza nguvu ktk ukusanyaji.
- Aidha menejiment inaendelea kukusanya na kurekebisha changamoto za ubovu wa Magari yaliyopo ili yaweze kusogeza majukumu yake.

Wajumbe waliipokea taarifa ya mapato na matumizi na kuijadili mwisho walitoa ushauri kwamba wakuu wa idara washirikiane na ofisi ya Mweka Hazina kuona namna ya kukusanya fedha za mapato ya ndani.

**FUM. MUHT. NA. 7/12/2021/2022: MAPENDEKEZO YA KUTUMIA SERIKALI ZA VIJIJI KUKUSANYA MAPATO YA HALMASHAURI.**

Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara aliwasilisha Mapendekezo ya kutumia serikali za vijiji kukusanya mapato ya Halmashauri ambapo kutokana na sababu zifuatazo Halmashauri imeleta mapendekezo ya kutumia serikali za vijiji kukusanya mapato. Sababu hizo ni:-

- Kuwapa nafasi wataalam wanaokusanya kwa sasa waendelee na majukumu yao ya kitaalamu.
- Asilimia tunayoirudisha kwa wakusanyaji iweze kwenda moja kwa moja vijijini, hivyo kupunguza malipo ya asilimia kulipa mara mbili.
- Kwa kuwa serikali za vijiji ndio huelewa hali halisi ya eneo walilopo hivyo itapelekea kusaidia kuzuia utoroshaji wa mapato kwa kudhibiti kwa ukaribu zaidi.
- Pia itapelekea kuongeza asilimia ya mapato vijijini kwani serikali za vijiji zinahitaji kuongeza mapato kwa ajili ya kuendeleza majukumu yao.
- Kupunguza gharama za ukusanyaji kwa kutoa wataalam kutoka makao makuu kwenda maeneo husika.
- Kwa vile vijiji vitanufaika moka kwa moja na asilimia hivyo itawawezesha kupata moyo wa kuibua vyanzo vipya vya mapato.

Wajumbe waliipokea taarifa na kuijadili mwisho walitoa ushauri kama ifuatavyo.

- Idara ya Ardhi na Maliasili wajitahidi ili kuhakikisha kuwa wanaongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kupitia vyanzo walivyonavyo.
- Idara ya Kilimo wahakikishe kuwa wanamfuatilia mzabuni ambaye anataka kulima kwenye mashamba ya Mkuyu na Mbwego ili aweze kufanya malipo na hivyo kuongeza mapato ya ndani.

Mwisho wajumbe waliipitisha taarifa.

**CMT. MUHT. NA. 8/12/2021/2022: MCHANGANUO WA FEDHA ZA UVIKO 19**

Mkuu wa Idara ya Mipango aliwasilisha taarifa kuwa Halmashauri imepokea fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha Tshs.4,733,231,075.51 kwa amchanganuo ufuatao. Ujenzi wa zahanati ya Kwamaligwa Tshs.50,000,000/=, ujenzi wa zahanati ya Mbogo Tshs.50,000,000/= , ujenzi wa zahanati ya Mnkonde Tshs.50,000,000/=, ujenzi wa nyumba mganga Tshs.90,000,000/=, ujenzi wa Emergency Medical Department

Tshs.300,000,000/= , ujenzi wa Maabara Kikunde sekondari Tshs.30,000,000/=, ujenzi wa maabara Pagwi sekondari Tshs.30,000,000/= ujenzi wa maabara Jaila sekondari Tshs.30,000,000/= Ujenzi wa maabara Mafisa sekondari Tshs.30,000,000/=, ujenzi wa maabara Mkindi Skondari Tshs.30,000,000/=, fedha za chanjo awamu ya pili Tshs.36,731,075.51, ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye uhitaji maalum Tshs.80,000,000/=, fedha za ufuatiliaji wa miradi Tshs. 6,500,000/= , ujenzi wa madarasa 65 katika shule za sekondari Tshs.1,300,000,000/=, ujenzi wa madarasa 131 katika vituo shikizi 43 Tshs.2,620,000,000/=
Wajumbe waliipokea taarifa na kuijadili kisha waliipitisha.

**CMT. MUHT. NA. 9/12/2021/2022: TAARIFA YA KUANZISHA KITUO CHA MATANGAZO YA REDIO KWA UFADHILI WA MFUKO WA MAWASILIANO KWA WOTE.**

Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA aliwasilisha taarifa kuwa Halmashauri inatarajia kuanzisha kituo cha matangazo ya redio kwa ufadhili wa mfuko wa mawasiliano kwa wote ambapo Halmashauri iliomba ufadhili katika Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF), kituo hiki kitamilikwa na Halmashauri kama kampuni ya Halmashauri na kinatarajia kuansihwa kwa ufadhi wa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF) kwa wastani wa gharama ya kiasi cha Tshs.250,000,000 kwa mchanganuo ufuatao.
Mitambo ya matangazo Tshs.168,420,000.00, vifaa vya ofisi Tshs.14,400,000.00, samani za ofisi Tshs.7,920,000.00, vifaa vya ujenzi Tshs.3,000,000.00, ufundi na mhandisi Tshs.48,435,000.00, leseni ya kumiliki kituo cha matangazo ya redio Tsh.8,000,000.00. Jumla kuu Tshs, 250,175,000.00
Wajumbe waliipokea taarifa na kuijadili mwisho waliipitisha.

**CMT. MUHT. NA. 10/12/2021/2022: TAARIFA YA UTOAJI WA MIKOPO.**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii aliwasilisha taarifa kuwa timu ya menejimenti katika kikao vhake cha tarehe 15.12.2021 ilipokea na kujadili mapendekezo ya mikopo kutoka kamati ya huduma za mkopo ya Wilaya yenye thamani ya Tshs.287,737,000/= kutoka kwa vikundi 21 vya wanawake na vijana. Timu ilipendekeza mikopo yenye thamani ya Tshs.112,500,00/= kwa vikundi 21 ( 15 vya wamawake na 6 vya vijana).

Wajumbe waliipokea taarifa na kuijadili kisha waliipitisha.

**CMT. MUHT. NA. 11/12/2021/2022:MENGINEYO.**

- Menejimenti iangalie njia bora ya kunusuru vifaa vya kielektroni ndani ya ofisi za Halmashauri kutokana na kuungua kila mara kunakosababishwa na jenereta la Halmashauri kila mara linapowashwa.
- Watumishi wahimizwe kufanya mapitio ya taarifa zao za OPRAS kwa nusu mwaka.

**CMT. MUHT. NA. 12/12/2021/2022: KUFUNGA KIKAO.**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti aweze kufunga kikao baada ya agenda zilizowasilishwa kukamilika. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kisha alifunga kikao majira ya saa 8:58 alasiri

**UMETHIBITISHWA:**

| KATIBU | MWENYEKITI |
|---|---|
| JINA. RASHID ABEID | JINA. GRACIAN MAKOTA |
| CHEO. Pg. DHRO | CHEO. DED |
| SAHIHI. [signature] | SAHIHI. [signature] |

11.1.2022

**TAREHE**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAMATI YA MENEJIMENTI CHA TAREHE 15.12.2021.**

| NA. | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| CMT. MUHT. NA. 5/12/2021/2022 | Kuhusu suala la matundu ya vyoo katika shule ya Msingi Ngeze wajumbe waliziagiza idara za Elimu Msingi, Mipango, Ujenzi pamoja na Kitengo cha Manunuzi wakakae na wahusika ili kuona namna bora ya kufanya ili kukamilisha mapungufu yaliyojitokeza kwa ajili ya kufuta hoja hii. | DPEO, DPLO, DE na HPMU | Ufuatiliaji umefanyika na kukuta marekebisho mengi yamefanyiwa kazi kwa lengo la kukamilisha mradi wa ujenzi huu wa choo. |